**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA**

**MTIHANI WA STASHAHADA YA UALIMU WA SEKONDARI**

**711** **KISWAHILI**

**Muda: Masaa 3** **Ijumaa, 01rd May 2015 Asubuhi**

**Instructions.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali kumi na sit (16).
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali mawili kutoka kila sehem **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na sehemu **B** na **C** Zina jumla ya alama **sitini (60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha majibu.

maktaba.tetea.org
TETEA



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali yote katika sehemu hii. Kila swali kina alama 4.

1. (a) Eleza maana ya lugha ya taifa.
   (b) Taja sababu mbili zinazofanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa nchini Tanzania.
   (c) Eleza tofauti kati ya lugha ya taifa na lugha ya kimataifa.
   (d) Kwa nini ni muhimu kuitunza na kuiendeleza lugha ya taifa?

2. (a) Eleza maana ya sentensi changamano.
   (b) Tunga sentensi moja ya changamano ukitumia kiunganishi *ingawa*.

3. Toa maana ya mofimu na eleza tofauti kati ya mofimu huru na mofimu tegemezi kwa kutoa mfano mmoja kwa kila aina.

4. Taja ngeli mbili za nomino na andika sentensi moja kwa kila ngeli uliyoitaja.

5. Eleza maana ya kivumishi na taja aina mbili za vivumishi ukitunga sentensi moja kwa kila aina.

6. (a) Fafanua maana ya methali.
   (b) Taja methali mbili zinazofundisha umuhimu wa juhudi na subira.

7. Eleza maana ya tamathali ya usemi ya tashbihi na andika sentensi moja yenye tashbihi.

8. (a) Eleza maana ya fasihi simulizi.
   (b) Taja aina mbili za fasihi simulizi na eleza sifa moja ya kila moja.

9. Kwa hoja mbili, eleza namna lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika kukuza utamaduni wa Mtanzania.

10. Eleza hoja mbili zinazothibitisha kuwa matumizi ya Kiswahili katika nyanja za teknolojia ni muhimu kwa maendeleo ya taifa.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali mawili kati ya manne. Kila swali lina alama 15.

11. Eleza kwa hoja sita umuhimu wa kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia katika shule za sekondari.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

12. Kwa hoja sita, jadili mchango wa mashairi ya Kiswahili katika kukuza maadili mema katika jamii.

13. Toa hoja sita zinazoonyesha jinsi mitandao ya kijamii inavyoweza kuchochea au kuathiri matumizi sahihi ya Kiswahili miongoni mwa vijana.

14. Eleza kwa hoja sita jinsi elimu ya lugha ya Kiswahili inavyoweza kutumika katika kujenga ajira na ujasiriamali nchini Tanzania.

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali mawili tu kutoka sehemu hii. Kila swali lina alama 15.

15. Andika insha ya hoja yenye kichwa: *Umuhimu wa kuhifadhi fasihi simulizi katika kizazi cha sasa.*

16. Eleza kwa hoja sita namna ambavyo mafunzo ya Kiswahili yanavyoweza kuboresha mawasiliano katika sekta za umma na binafsi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org